



Malaika Angels

Mary Baker Eddy

Miscellaneous Writings, ukrasa 306

Wakati ambao malaika wanatutembelea, sisi hatusikii chakacha ya mabawa, wala kuhisi mgusano wa manyoya ya kifua cha njiwa; lakini tunajua kuwa wako hapo kwa ajili ya upendo wanaoleta mioyoni mwetu. Aha! Laiti ungesikia mgusano *huu*, — siyo kushikana mikono, wala mtu mpendwa kuwepo; ni zaidi ya hii: hili ni wazo la kiroho linaloangazia njia yako! Mtungaji wa Zaburi hunena: “Yeye atakuagizia malaika Zake.” Mungu hukupa mawazo Yake ya kiroho, nayo yanakupa mahitaji yako ya kila siku. Usiulize ya kesho kamwe: yatosha kuwa Pendo takatifu ni msaada uliopo nyakati zote; na iwapo utangoja, bila wasiwasi, utapata vitu vyote unavyohitaji kila wakati. Si huu ni urithi mtukufu ajabu kupita kiasi tunaopewa kwa njia ya ufahamu wa Pendo iliyopo kila mahali nyakati zote! Hatuwezi kuomba zaidi. Zaidi ya hayo hatutaki: Zaidi ya hayo hatuwezi kuwa nayo. Hakikisho hili tamu ndilo “Amani, tulia” kwa hofu zote za binadamu, na taabu za aina zote.

For this translation in English and other translations in Swahili, please see <http://translations.christianscience.com>

Translation © 2010 The Christian Science Publishing Society

This translation has been performed by Mother Church members in the Field and made available by agreement with The Christian Science Publishing Society. You may reproduce up to 100 print copies of this Article. You may not sell or reprint this Article in another publication without permission of CSPA. You may not post or embed this Article on other websites; instead please link to the Article on the CSPA website.